

## **KANUNI NA TARATIBU ZA KILIMO BORA CHA ZAO LA MBAAZI**

### ***Zao la mbaazi.***

#### ***utangulizi***

Mbaazi za muda mfupi hukomaa kati ya siku 120 hadi 125 katika maeneo ya Morogoro, Tanga, Pwani, na Dar es Salaam. Mbaazi hizi hukomaa kwa siku 120 tu. Katika ukanda wa juu kwenye baridi, mbaazi za muda mfupi hukomaa kwa muda mrefu zaidi ya siku 120. Mbaazi za kienyeji hukomaa kati ya siku 210 hadi 270. Mbaazi za muda mfupi hutoa mazao mengi zaidi ya zile za kienyeji iwapo zitalimwa kwa kuzingatia maelezo yaliyomo humu.

#### **Aina**

Mbaazi aina ya komboa imefanyiwa utafiti na Kituo cha Utafiti Ilonga Kilosa na kuonekana nzuri zaidi na kwamba kituo kinazalisha mbegu hizo.

#### **Wakati wa kupanda**

Mbaazi za muda mfupi zinaweza kupandwa wakati wa masika au mvua za vuli za kuaminika za ukanda wa Pwani.

#### **Nafasi ya kupanda**

Panda kwa umbali wa Sentimita 50 kati ya mistari na Sentimita 20 kati ya mashina. Panda mbegu 3 kila shimo. Wiki mbili baada ya kuota, punguza mmea mmoja ili ibaki miwili kwa kila shina. Usichanganye na mazao mengine.

#### **Palizi**

Hakikisha shamba linakuwa safi kwa kupalilia mara kwa mara katika wiki 6 za mwanzo. Baada ya hapo palilia tu inapobidi kufanya hivyo.

#### **Dhibiti ya wadudu.**

Mbaazi za muda mfupi hushambuliwa sana na wadudu. Nyunyiza dawa ya kuua wadudu mara tu zinapoanza kutoa maua hadi kukomaa. Dawa zinazofaa ni karate, Thiodan, Rogor, Decis, Ripcord au nyingine utakayoshauriwa na mtaalam wa kilimo.

#### **Uvunaji**

Vuna wakati mbaazi zimekomaa vizuri vitumba vinapobadilik kuwa na rangi ya kahawia. Vuna kila baada ya siku 3 hadi 5 kwa kuchuma vitumba au kukata matawi. Kausha juani, piga na kupeta.

### **Kiasi cha mavuno na hifadhi**

Mbaazi za muda mfupi hutoa kilo 600- 800 ( magunia 6-8 kwa ekari au kilo 1500 hadi 2000 kwa hekta kama zimetunzwa kwa kufuata maelekezo yaliyomo humu. Mbaazi zilizokauka vizuri huhifadhiwa kwa kutumia madawa aina Actellic super dustgram 100 kwa gunia la kilo 100.